

# Jinsi ya Kulinda Afya ya Mtoto wako na Yako Mwenyewe Iwapo Umeambukizwa Homa ya Manjano B na Wewe ni Mjamzito

Homa ya manjano B ni ugonjwa hatari ambao mwili wako unaweza kubeba milele. Iwapo wewe ni mjamzito na umeambukizwa homa ya manjano B, virusi hivyo vinaweza kuambukiza mtoto wako kupitia mgusano na damu yako wakati wa kuzaliwa. Ili kuzuia maambukizo kwa mtoto wako na wewe mwenyewe kuwa na afya nzuri, tembelea mhudumu wa afya mapema wakati wa ujauzito wako na uongee na wao kuhusu homa ya manjano B.



**Tumia jedwali hili kufuatilia utunzaji wako na utunzaji wa mtoto wako wakati wa na baada ya ujauzito!**

## Ya Mama

### Wakati wa Ujauzito

- ✓ Tembelea mhudumu wa afya kwa ajili ya utunzaji wa homa ya manjano B mapema katika ujauzito wako ili kuangalia kiwango chako cha homa ya manjano B na utendakazi wa ini lako.
  - Mhudumu wako wa afya anaweza kupendekeza dawa za homa ya manjano B, iwapo zinahitajika.

### Wakati wa Kuzaa

- ✓ Hakikisha wafanyakazi katika hospitali wanajua kuwa una homa ya manjano B.
- ✓ Hakikisha kuwa mhudumu wa afya atakayemtunza mtoto wako anajua kuwa una homa ya manjano B.

### Baada ya Kuzaa na Baadaye

- ✓ Katika miezi 1-2, fuatilia na mhudumu wako wa afya ili upate utunzaji wa homa ya manjano B.
  - Hii ni muhimu hasa iwapo ulianza matibabu wakati wa ujauzito.
- ✓ Fuatilia na mhudumu wako wa afya kwa ajili ya ufuatiliaji wa homa ya manjano B angalau kila baada ya miezi 6.

## Kwa Mtoto

### Wakati wa Kuzaa

- Mtoto lazima apokee chanjo 2 ndani ya saa 12 baada ya kuzaliwa ili kumlinda dhidi ya kuambukizwa:
- ✓ Dozi moja ya chanjo ya globulini ya kingamwili ya homa ya manjano B (HBIG)
  - ✓ Dozi ya 1 ya chanjo ya homa ya manjano B

### Miezi 1-2

- ✓ Mtoto wako apokee chanjo yao ya 2 ya homa ya manjano B.

### Miezi 6

- ✓ Mtoto wako apokee chanjo yao ya 3 ya homa ya manjano B.

### Miezi 9-12

- ✓ Mtoto wako anahitaji kipimo cha damu ili kuangalia hali yao ya homa ya manjano B na kutathmini kiwango chao cha kinga.

## Kunyonyesha

- ✓ Ongea na mhudumu wako wa afya kuhusu msaada wa kunyonyesha na jinsi ya kuzuia au kudhibiti chuchu zilizopasuka au zinazotoa damu ili kupunguza mgusano wa mtoto na damu yako.
- ✓ Iwapo mtoto aliyezaliwa amepokea chanjo ya homa ya manjano B na kingamwili ya globulini ya homa ya manjano B wakati wa kuzaliwa, hatari ya msambao wa homa ya manjano B wa mama kwenda kwa mtoto kupitia kunyonyesha utakuwa chini sana. Mara tu mtoto wako amepokea chanjo hizi, ni salama kumyonyesha.



**Hakikisha mchumba wako na wanaoishi na wewe wamepimwa na wamepokea chanjo ya homa ya manjano B wakati wa ujauzito wako.**